Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: Watu wa aina tatu mimi ndiye mgomvi wao siku ya Kiyama

Imepokelewa kutoka kwa Abuu Huraira radhi za Allah ziwe juu yake kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake amesema: "Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: Watu wa aina tatu mimi ndiye mgomvi wao siku ya Kiyama: Mtu aliyetoa (kiapo) kwa jina langu kisha akafanya usaliti, na mtu aliyemuuza mtu huru kisha akala thamani yake, na mtu aliyempa kazi mwajiriwa, akatimiza majukumu yake na hakumpa malipo yake".

[Sahihi] [Imepokelewa na Al-Bukhaariy]

Ameeleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake ya kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: Watu wa aina tatu mimi ndiye nitakayepambana nao siku ya Kiyama, na nitakayekuwa mgomvi wake basi nitapambana naye na kumshinda: Wa kwanza: Atakayetoa kiapo na akaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, na akachukua ahadi kisha akaitengua na kufanya hiana. Wa pili: Atakayemuuza mtu huru kwa kumfanya kuwa mtumwa na akala thamani yake na akakitumia kiwango cha pesa aliyopata. Wa tatu: Atakayemuajiri muajiriwa katika kazi, akamtimizia kazi yake na hakumpa thamani ya kazi yake.

http://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/66163